

# **Uzingativu wa Vipengele vya Kimuundo kama Inavyoakisiwa katika Tafsiri za Awali katika Kiswahili na Lugha za Kibantu**

*Pendo S. Malangwa*

## **Ikisiri**

Mara nyingi nadharia za tafsiri zinasisitiza uzingatiaji wa maudhui katika matini huku zikitupilia mbali masuala ya kimuundo ambayo pia ni muhimu katika aina fulani za matini zinazotafsirwai. Tafsiri za awali katika Kiswahili na lugha za Kibantu nchini Tanzania zimeakisi suala la uzingatiaji na umuhimu wa vipengele vya kimuundo katika uhawilishaji wa maudhui ya matini husika. Tafsiri za awali hapa ina maana ya tafsiri zilizofanya na wamisionari, wakoloni na baadhi ya wazungumzaji wa lugha ya Kiswahili wakati wa ukoloni na kipindi kifupi baada ya uhuru. Makala haya yanakusudia kuehambua na kuainisha vipengele vilivyoahawilishwa katika matini hizi kutoka katika matini za lugha chanzi. Aidha, yataonesha na kusisitiza umuhimu wa kuzingatia vipengele vya kimuundo katika tafsiri za aina mbalimbali za matini. Lengo la makala haya si kurejesha nyuma mjadala ambao umekuwepo kwa muda mrefu juu ya kipi muhimu kati ya maudhui au vipengele vya kimuundo katika tafsiri, bali ni kubainisha kwamba, pamoja na msisitizo mkubwa wa kuzingatia maudhui, vipengele vya kimuundo pia ni muhimu katika kufanikisha uhawilishaji wa maudhui hayo. Matini zitakazorejelewa ni matini za kifasihi, kidini na za masomo maalumu, hasa zilizotafsiriwa kabla ya miaka ya 1980 na wamisionari, wakoloni na baadhi ya wazungumzaji wa lugha ya Kiswahili na lugha nyingine za Kibantu. Masuala yatakayochambuliwa ni pamoja na vipengele vya kisanaa, muundo na mtindo. Data itachambuliwa kwa kutumia mkabala wa ulinganishaji kati ya matini ya lugha chanzi na ile ya lugha lengwa.

## **1.0 Utangulizi**

Tafsiri za awali katika Kiswahili na lugha nyingine nchini Tanzania zina mchango mkubwa sana katika jamii ya Watanzania. Sambamba na kuwasaidia kujifunza mbinu za tafsiri, zilisaidia kuboresha na kujifunza mbinu za uandishi na usanii mpya. Kauli hii inaakisi ukweli kwamba tafsiri za awali hazikufanywa na Watanzania. Kama anavyofafanua Mojola (1999), tafsiri za awali zilifanywa na wakoloni na wamisionari, japokuwa baadae waliwahusisha wenyeji. Mojola anaendelea kufafanua kwamba wamisionari walipokuwa hapakuwa na maandiko yoyote kuhusu au katika Kiswahili na lugha nyingine za watu waliokuwa wakiishi katika eneo hili. Wageni hawa walipokuwa walifanya utafiti kuhusu lugha hizi ili kujifunza sarufi yake na kuanda orodha ya maneno. Waliandika pia vitabu vya sarufi, kamusi na tafiti maalumu zinazofafanua masuala tatanishi ya kisarufi (Mwita, 2008). Kwa misingi hiyo basi, wageni hawa ndio walioiingiza taaluma hii ya tafsiri nchini Tanzania na katika maeneo mengine ya Afrika Mashariki. Lengo kuu lilikuwa kufanikisha shughuli zao kupitia mawasiliano ambayo yalifanyika katika lugha za wenyeji. Hivyo basi, tafsiri hizi ziliikuwa ni chachu ya kujifunza masuala mbalimbali yanayohusiana na lugha, fasihi na tafsiri.

## 2.0 Kanuni Muhimu katika Tafsiri za Awali

Ni vyema katika makala haya kudokeza hatua muhimu walizosuata wafasiri wa awali katika kufanikisha zoezi la kutafsiri kwenda katika Kiswahili na lugha nyingine za Kiafrika. Mjada la huu utakitwa zaidi kwa wafasiri wamisionari kwani wao ndio waliosanya kazi kubwa ya kuandika miongozo mbalimbali ya kuwasaidia wafasiri wa wakati huo, ambayo pia inafaa kuzingatiwa hata wakati huu. Kwanza kabisa wafasiri wa awali walijiwekea kanuni muhimu za kuzingatia wakati wote wa zoezi la kutafsiri. Ohly (1975) anaorodhesha kanuni zifuatazo:

1. Lugha inayotumika sharti iwe inaeleweka kwa kila mtu, bila kujali kiwango chake cha climu;
2. Mtindo lazima uwiane na maudhui/ujumbe pamoja na madhumuni/ malengo ya kazi husika;
3. Ujumi wa lugha sharti uzingatiwe na/ au udumishwe; na
4. Wafasiri wanaruhusiwa kurahisisha baadhi ya mambo ili kueleza vyema maudhui ya matini husika na kuwasaidia wasomaji wote waelewe.

Kwa kuwa wafasiri walikuwa na lengo la kufanikisha upelekaji wa injili, kanuni hizi ziliwekwa kwa lengo la kuwaongoza wafasiri kutoa tafsiri rahisi na inayoelewaka. Dammann (1977) anafafanua kwamba wafasiri walijitahidi sana kuweka uwiano wa lugha ili kuwasaidia wasomaji wa Biblia, wasomi na wasio wasomi. Pamoja na msisitizo huu wa kurahisisha na kutumia lugha inayoelewaka kwa kila mtu, masuala ya kimuundo hayakufutiliwa mbali. Haya pia yaliwekewa kanuni yake maalumu (tazama, kanuni ya 2 na 3 hapo juu). Hapa msisitizo ni kwamba, wafasiri waheshimu vipengele vya kimuundo vinavyoitambulisha matini husika ili kutoa matini ya Lugha Lengwa (I.L.) yenye uwiano na matini chanzi. Uzingatiaji wa vipengele vya kimuundo katika tafsiri za awali unajadiliwa kwa kina katika sehemu inayosuata.

## 3.0 Uzingativu wa Vipengele vya Kimuundo

Wafasiri wa awali katika Kiswahili na lugha nyingine za Kibantu, pamoja na masuala ya kimaudhui, walizingatia sana vipengele vya kimuundo kutegemeana na aina ya matini husika. Vipengele vya kimuundo vitakavyojadiliwa hapa ni umbo la matini, lugha ya kisanaa na masuala ya kiistilahi. Tafsiri za awali katika Kiswahili na lugha nyingine za Kibantu zina mambo kadhaa ambayo wafasiri wachanga wanaweza kujifunza ili kukuza uwezo wao katika kutekeleza zoezi la tafsiri. Baadhi ya masuala haya yanafafanuliwa hapa chini:

### 3.1 Umbo la Matini

Umbo la matini ni kipengele muhimu sana katika kubainisha aina fulani ya matini. Mathalani, ushairi unabainishwa kwa kuangalia umbo lake la kiubeti, mistari misupi mifupi, lugha ya mkato, uwepo wa urari wa vina na mizani, na kadhalika. Riwaya kwa kawaida huwa katika umbo la kinathari (masimulizi), aya na sura mbalimbali. Tamthiliya, kwa upande mwagine, hubainishwa na uwepo wa majibzano (dialoja)

baina ya wahusika wake, sehemu za maonyesho au mgawanyiko wa schemu za igizo. Kwa misingi hiyo, mfasiri anapokabiliwa na zoezi la kutafsiri aina fulani ya matini hulazimika kuhawilisha pia umbo la matini hiyo. Kwa mfano, anapofasiri shairi hulazimika kufasiri ubeti mmoja mmoja na kujitahidi hata kuibua vina na mizani katika matini lengwa. Kamwe, haikubaliki kufasiri umbo la ushairi kinathari. Wafasiri wa Maandiko Matakatifu, Biblia kwa mfano, pamoja na changamoto ya kuwepo kwa maumbo mbalimbali ya aya na sura za Biblia walijitahidi sana kuzingatia umbo la kila kitabu walichokishughulikia. Ikiwa kitabu husika kimewasilisha maudhui yake kiushairi, wafasiri pia walijitahidi kuiga umbo hilo katika lugha lengwa. Hebu tutazame tafsiri zisuatazo za kitabu cha Zaburi katika Kiswahili na Kihaya (Zaburi 147: 1-2):

Mfano 1:

**Kiingereza kama Lugha Chanzi (LC<sup>1</sup>)**  
*Hallelujah.*  
*How good it is to sing praises of our God,*  
*How Pleasant and fitting to praise Him!*  
*The Lord builds up Jerusalem;*  
*He gathers the exiles of Israel.*  
 (The Holy Bible, 1973)

**Kiswahili kama Lugha Lengwa (LL)**  
*Haleluya.*  
*Msituni Bwana;*  
*Maana ni vema kumwimbia Mungu wetu,*  
*Maana kwapendeza, kusifu ni kuzuri.*  
*Bwana ndiye ajengaye Yerusalem,*  
*Huwakusanya waliotawanyika wa Israel.*  
 (Biblia, Maandiko Matakatifu, 1997)

#### **Kihaya - LL**

*Haleluya;*  
*Kuba kirugi kuhoyerwa Katondo waitu;*  
*Eego, kishemera, kandi kisaine kumuhausikiliza.*  
*Rubaho niwe ayombeka Yerusalem;*  
*Ashombokya hamoi Abaisrael abanamagirwe.*  
 (Endagano Empya N'Zaburi, 1968/1972)

Katika kuzitazama tafsiri hizi, hata kama ni kwa haraka haraka, inaonesha kwamba tafsiri hizi zimezingatia umbo la kishairi la matini chanzi. Usomaji wa tafsiri za Biblia unaonesha kwamba, wafasiri walikuwa makini katika kuhawilisha maandiko haya kwa kuzingatia umbo lake. Hii ina maana kwamba, pale ambapo Biblia ya lugha chanzi (yaani, LC) iliandikwa kinathari au kishairi, tafsiri pia iliigiza umbo hilo. Katika kupitia Biblia, katika vitabu vya Agano Jipya, inaonesha kwamba wafasiri walizingatia umbo la matini hizi ili kudumisha mguso, imani ya wasomaji na vionjo vyake. Tazama mfano ufuatao kutoka katika kitabu cha Marko (Marko 1: 1-4):

<sup>1</sup> Neno "kama" linatumika kuashiria kwamba tafsiri za awali, na hasa za kidini, zimefanywa kutoka lugha mbalimbali kama Kigiriki au Kiyunani. siyo Kiingereza wakati mwagine.

## Mfano 2:

### **Kiingereza kama LC**

*The beginning of the gospel about Jesus Christ, the Son of God. It is written in Isaiah the prophet:*

"I will send my messenger ahead of you.  
Who will prepare your way?"  
"A voice of one calling in the desert,  
'Prepare the way of the Lord.  
Make straight path for him.'"

*And so John came, baptizing in the desert region and preaching a baptism of repentance for the forgiveness of sins.*

(The Holy Bible, 1973)

### **LL – Kihaya**

*Embandizo y'Evangeli ya Yesu Kristo, Omwana wa Katondo, nk'okwo kyahandiikirwe omu murangi Yesaya kiti:*

*Leeba, nintuma entunwa yange omu maisho gaave.  
Aliteekateeka omuhanda gwave.  
Eiraka ly'alikugambira eiguru omu irungu liti:  
Muhangule omuhanda ng'Omukama.  
Mugorole otuhanda twe!*

*Yohana Omubatiza akaboneka omu irungu, naaranga omubatizo ng'okweechuza n'okuhindura emitima, kugarulirwa amafu.*

(Endagano Empya N'Zaburi, 1968/1972)

Data iliyowasilishwa hapo juu imeonesha umakini wa mfasiri katika kuzingatia muundo wa matini chanzi. Imebainika kwamba mfasiri amejitahidi kulihawilisha umbo kama linavyojitokeza katika matini chanzi. Kwa mfano, lugha ya kinathari imewasilishwa kinathari na lugha ya kishairi kadhalika. Kukiuka umbo la matini chanzi yoyote ambayo mfasiri anaishughulikia ni sawa na kutunga kitu kipyta, kama alivyofanya J. K. Nyerere katika tenzi zake za vitabu vya Injili. Hebu tazama Marko 1 :1-4 iliyowasilishwa na Nyerere (1996):

## Mfano 3:

- |  |  |
|--|--|
| 1. Awali utangulizi<br>Wa haya masimulizi<br>Ya injili ya Messia<br>Yesu Mwana wa Jalia .... | 3. Na sauti ya nyikani<br>Italia : Tengenezeni<br>Mapito yake Manani<br>Njia zake zinyosheni |
| 2. Kama alivyoandika<br>Nabii wake Rabuka.<br>Isaya akialika:<br>Angalia namtuma             | 4. Basi Nabii yohana<br>Alikuwako nyikani<br>Akibatiza kauma<br>Na kuhubiri kwa wema         |

Malaika wangu mwema.  
Kwenda kututangulia.  
Na kutunyoshea njia.

Ubatizo wa kutubu  
Na kwondolewa dhunubu.

Kinachooneckana katika utungo huu wa Nyerere ni kitu kipyta japokuwa kina maudhui yanayowiana na maudhui ya mafungu ya Biblia. Mafungu ya Biblia na tafsiri zake yapo katika muundo wa nathari. Tenzi za Nyerere ziko katika umbo la kishairi. Hiki ndicho wanachosisitiza Savory (1968), Mapaje na White (1983), Mwansoko na wenzake (2006) kuwa kufanya hivyo ni sawa na kutunga kitu/shairi jipya. Kwa hakika, Nyerere alichofanya ni kutunga kitu kipyta na ndio maana anaita tenzi na siyo vitabu vya injili kama inavyosawiliwa katika Biblia.

Aidha, tafsiri kama za nyimbo za kidini zilizofasiriwa katika lugha mbalimbali za Kibantu, kikiwamo Kisukuma zimezingatia umbo na mahadhi ya matini chanzi. Hebu tazama data ifuatayo:

Mfano 4 :

**Kiingereza kama LC**

Refrain  
*Peace, peace, wonderful peace,  
Coming down from the father  
Above;  
Sweep over my spirit forever, I pray,  
In fathomless billows of love.*

*What a treasure I have in this wonderful peace.  
Buried deep in my innermost soul.  
So secure that no power can mine it away,  
While the years of eternity roll.*  
(Church Hymnal, 1985)

**Kisukuma - LL**

*Mhola, mhola ninge  
Mhola ya Yehova Mulungu,  
Twanumba Mulungu shigu welelo  
Kulwa ndena mhola mu Yesu*

*Mhola ninge ntenayo mu moyo gwane  
Mhola ya Yehova Mungungu  
Mulugendo lwa muse ekundindaga  
Ndenako kwifura mu Yesu*

Wimbo huu, na nyimbo nyingine za kidini tunazozifahamu zimefasiriwa katika lugha mbalimbali na zinaiimbika kwa mahadhi sawa katika lugha zote. Kadhalika, maudhui yake yanawiana kati ya tafsiri ya lugha moja na nyingine. Japokuwa mhakiki wa tafsiri ya wimbo huu anaweza kubaini marekebisho fulani katika baadhi ya vipengele lakini maudhui na vipengele vingi vya kimuundo huzingatiwa ili kutoa vionjo vinavyowiana baina ya LC na LL. King'ei (2002) anafafanua kwamba ingawa tafsiri inaweza kuonekana kama aina mojawapo ya sayansi ya lugha, lakini pia ni usanii kwa maana kwamba daima mfasiri huongozwa na milango ya fahamu kuliko kanuni na sheria. Kwa kufanya hivyo, wafasiri daima huingiza ujuzi/maarifa yao na hata uzoefu wao. Mambo haya yote humsaidia mfasiri kutoa tafsiri kubalifu na inayowiana na matini ya LC. Tazama pia mfano ufuatao katika Kiswahili:

Mfano 5:

**Kiingreza kama LC**

*All to Jesus I surrender,  
All to Him I freely give;  
I will ever love and trust Him,  
In His presence daily live;*

*Refrain*

*I surrender all,  
I surrender all;  
All to Thee, my blessed Savior,  
I surrender all.*

(Church Hymnal, 1973: 309)

**Kiswahili - LL**

Yote namtolea Yesu  
Nampa moyo wote,  
Nitampenda siku zote,  
Namwandama kila saa.

Yote kwa Yesu,

Yote kwa Yesu,  
Yote Kwako, Ee Mwokozi,  
Natoa sasa. (Pia *Yote kwa Yesu*)  
(Tenzi za Rohoni, 1968: 52)

Katika mfano huu inaonekana wazi kuwa mfasiri amezingatia umbo la matini chanzi katika kuhawilisha ujumbe katika LL. Mzungumzaji wa LC anaposimama kuimba wimbo au ushairi huu na mzungumzaji wa LL huimba kana kwamba wanaimba kwa lugha moja. Hakuna anayejisikia kupwaya kwa mwenzake. Hali hii hujitokeza katika makanisa yanayotumia lugha mbili au zaidi. Waumini wake huwa na vitabu vya nyimbo vya lugha mbalimbali na hujisikia kana kwamba wanatumia kitabu cha lugha moja. Ujuzi huu ni muhimu sana katika tafsiri za matini za aina mbalimbali. Wengine hudhani kwamba kufasiri ni kurahisisha kitu kigumu kilichoandikwa katika lugha fulani (yaani, LC).

### 3.2 Mbinu za Kisanaa

Mbinu za kisanaa ni muhimu sana katika kuitambulisha matini ya kifasihi. Kuidondosha mbinu mojawapo ya kisanaa ni kuinyima ujumi unaostahili tafsiri ya kifasihi. Kadhalika, kuongezea mbinu nyingine ya kisanaa ni kuitwisha mzigo wa ziada tafsiri inayotolewa, ambao matini ya LC haina. Mfasiri anashauriwa kuzingatia vipengele vya kisanaa viliviyotumika katika matini anayoishughulikia ili kutoa tafsiri inayowiana na matini chanzi yake. Wasomaji wa LL huwa na mategemeo makubwa wanaposoma tafsiri yoyote. Harries (1970) anabainisha makundi mawili ya wasomaji. Kwanza, kuna wale wanaosoma tafsiri kwa sababu hawajui LC na hivyo, wanasoma tafsiri yake ili kujua kinachozungumziwa katika matini hiyo. Pili, kuna wale wanaojua LC lakini wanasoma tafsiri ili ama kulinganisha na matini chanzi yake, kujifunza mbinu fulani alizotumia mfasiri fulani au kupima uwezo wa mfasiri katika kuhawilisha vipengele fulani vya matini husika, kama wafanyakyo wataalamu wengi wa tafsiri. Wafasiri wa awali, kama ilivyobainishwa hapo juu, walikuwa wakitungia hatua kadhaa kabla hawajahawilisha matini fulani, ikiwamo kubainisha istilahi au lugha maalumu na kuitafutia visawe katika LL. Hatua hii iliwasaidia kuhawilisha mbinu za kisanaa katika matini husika kwa umakini mkubwa. Tazama mfano ufuatao katika tafsiri ya Biblia katika Mathayo (5:1-10):

**Kiingereza kama LC**

--- His disciples came to him and he began to teach them, saying  
*Blessed are the poor in spirit,  
 For theirs is the kingdom of heaven.  
 Blessed are those who mourn,  
 For they will be comforted. ...  
 Blessed are those who hunger and thirst for righteousness,  
 For they will be filled....*

**Kiswahili - LL**

---wanafunzi wake walimjia,  
 akafumbua kinywa chake  
 akawafundisha akisema,  
 Heri walio masikini wa roho,  
 Maana ufalme wa mbinguni ni wao.  
 Heri wenye huzuni,  
 Maana hao watafarijika. ...  
 Heri wenye njaa na kiu ya haki,  
 Maana hao watashibishwa. ...

Katika matini hii kuna taswira ya sifa za watu wanaofaa kwa ufalme wa mbinguni, ambayo imekusudiwa wasomaji wa matini hii waipate. Tafsiri iliyotolewa imeakisi vyema taswira hii kwa wasomaji wa LL. Hebu tutazame pia tafsiri ya wimbo/ushairi ufuatao:

**Kiingereza - LC****Showers of Blessing**

*There shall be showers of blessing;  
 This is the promise of love;  
 There shall be season refreshing;  
 Sent from the savior above.  
 (Church Hymnal, 195)*

**Kisukuma - LL****Mbula ya Mbango Iliza**

*Mbula ya mbango iliza.  
 Mulungu wahaya We,  
 Ikanza lya lilubango,  
 Lyegela hangi mu si.  
 (Mimbo, 69)*

Hapa pia kuna taswira ya manyunu ya baraka kutoka juu, kwa muumba. Taswira hii imeakisiwa pia katika matini ya LL. Pamoja na kuwa mfasiri ametoa tafsiri pana (mvua badala ya manyunu) lakini amefanikiwa kwa kiasi kikubwa kuichora taswira ya mvua ya baraka inayongojewa kunyesha. Kwa kawaida baraka hazinyeshi lakini kwa sababu ya uwangi wake, mwandishi ametumia taswira ya mvua kuonesha kwamba baraka zinatoka juu na huwa ni nyingi mithili ya mvua.

Pale inapotokea mfasiri amekiuka kanuni hiyo, tafsiri yake hutambulika kama tafsiri finyu, tafsiri pana au hata tafsiri mbovu au isiyo sahihi (Malangwa, 2005; Mwansoko na wenzake, 2006; Newmark, 1988 na King'ei, 2002). Malangwa (itachapishwa karibuni) amejadili suala la tafsiri pana na tafsiri finyu katika tafsiri za kifasihi. Mathalani, kuhusu tafsiri finyu, Malangwa anafafanua kwamba tafsiri finyu hutokeea pale ambapo mfasiri anadondosha baadhi ya mbinu za kisanaa na kuzifasiri kwa maneno au lugha ya kawaida kama alivyofanya p'Bitek (1975), katika tafsiri ya *Wimbo wa Lawino*:

**Matini ya LC**  
*Maria the Clean Woman*  
*Mother of the Hunchback*  
*Pray for us who spoil things*  
*Full of graciya* (pg.115)

**Matini ya LL**  
*Maria Mtakatifu*  
*Mama wa Mungu*  
*Utuombee sisi wakosefu*  
*Uliyejaa Neema* (uk. 90)

Katika mfano huu, mfasiri amedondosha baadhi ya mbinu za kisanaa zilizotumika katika matini chanzi ambazo zimekusudiwa kuukejeli Ukristo. Tafsiri kama hii kwa ujumla imepwaya. Kwa ujumla, mfasiri wa matini za kifasihi anapaswa kuzingatia mbinu za kisanaa kwa lengo la kuwasaidia wasomaji wa matini lengwa ambao hitaji lao ni kupata kile kilichoandikwa katika LC kwa vionjo vinavyowiana na vile vya wasomaji wa LC.

### 3.3 Masuala ya Kiistilahi

Matini za kiufundi na matini za masomo maalumu kama vile sheria, dini na uchumi hubainishwa na matumizi ya rejestra fulani au istilahi fulani maalumu. Kwa mfano, istilahi kama vile *Mtume, Yehova, ushuhuda, Masihi, Mwokozi, Utatu Mtakatifu, Roho Mtakatifu, Kristo* (pia *Kristu*), *Allah, Issa bin Mariam na baraka* huhushwa na matini za kidini. Mfasiri yejote anapokabiliwa na matini ya uwanja maalumu anasisitizwa kutumia au kuunda istilahi zinazohusiana na uwanja husika. Wafasiri wa awali wa matini za kidini walikuwa makini katika kuunda na kutumia istilahi zinazoakisi uwanja husika. Katika uwanja wa dini kwa mfano, istilahi zifuatazo ziliundwa:

**Kiingereza kama LC**  
*Ark of the Covenant*  
*Holy Father*  
*Virgin Mary*  
*Association of the propagation of the Faith*  
*Acts of the Apostles*  
*Eternal life*  
*Holy Water*  
*Holy Scripture*  
*Kingdom of God*  
*Pastoral letter*  
*Ash Wednesday*  
*Heavenly Father*  
*(Tanzania Episcopal Conference<sup>2</sup>, 1965)*

**Kiswahili - LL**  
*Sanduku la Agano*  
*Baba Mtakatifu*  
*Bikira Maria*  
*Chama cha Kueneza Dini*  
*Matendo ya Mitume*  
*Uzima wa milele*  
*Maji ya Baraka*  
*Maandiko Matakatifu*  
*Ufalme wa Mungu*  
*Waraka wa kiaskofu* (pia, *Kichungaji*)  
*Jumatano ya majivu*  
*Baba wa Mbinguni*

Orodha hii ni istilahi za kidini katika LC na LL. Istilahi hizi pia ziliundwa kwa kuzingatia sarufi ya LL. Mkabala huu wa kubainisha istilahi maalumu na kuzitasutia

<sup>2</sup> Hizi ni Istilahi/Msamiati wa Kidini ambao ulichapishwa na *Tanzania Episcopal Conference* (1965); *Provisional Religious Vocabulary Swahili-English English-Swahili* katika *Swahili Journal of the Institute of Kiswahili Research*, Vol. 35/1, 77-95.

visawe vyake hutumika pia katika tafsiri za maandiko matakatifu katika lugha nyingine. Jitihada hizi za awali zimesaidia kutengeneza njia ya wafasiri wa sasa na wa baadae. Mathalani, Nyerere (1969) alipokuwa akitafsiri tamthiliya ya *Mabepari wa Venisi* aliweza kutoa tafsiri zifuatazo:

**Kiingrereza - LC**

This was a venture, sir, that Jacob served for  
A thing not in his power to bring to pass,  
But swayed and fashioned by the hand of heaven.  
(pg. 75)

**-Kiswahili - LL**

Bahati hii Yakobo aliifanya kazi,  
Kitu ambacho hakikuwa kwenye  
uwezo wake,  
Bali kilichofanyizwa kwa mkono wa  
mbinguni (uk.12).

Istilahi kama *mkono wa mbinguni, shetani- mtu, ibilisi* (uk.19), *Jumatatu-Nyeusi, Jumutano ya Majivu* (uk. 28), *baraka* (uk.13), *Mungu abariki* (uk.10), *msahafu, mtakatifu* (uk.14) ni za kidini. Nyerere alizipata istilahi hizi, bila shaka, kutoka katika uwanja huo wa dini ili kuweza kuhawilisha kwa usahihi dhana zilizokuwa zimewasilishwa katika matini ya LC. Hali hii imejitokeza pia katika tafsiri nyingine katika Kiswahili. Mathalani, Tafsiri ya *Wimbo wa Lawino* ya p'Bitek (1975) inahusisha tafsiri ifuatayo:

**Kiingereza - LC**

*Maria the Clean Woman*  
*Mother of the Hunchback*  
*Pray for us who spoil things*  
*Full of graciya* (pg. 115)

**Kiswahili - LL**

Maria Mtakatifu  
Mama wa Mungu  
Utuombee sisi wakosefu  
Uliyejaa Neema (uk. 90).

Tafsiri kama hii imezingatia muktadha wa matini za kidini. p'Bitek anapofasiri shairi lake anaelewa kwa usahihi kuwa katika muktadha wa kidini "Maria" si tu mwanamke (Woman) ila ni "Mama". Uelewa huu umemfanya akiuke hata lugha ya kisanaa iliyokuwa imetumiwa katika matini chanzi. Inawezekana mwandishi wa matini chanzi alikuwa anaelewa vyema namna ya kuandika kwa Kiingereza sahihi sala hiyo lakini kutohana na sababu za kuijumi ametumia 'Woman' badala ya 'Mother' na 'Hunchback' badala ya 'God'. Mfasiri pia alipaswa kutafuta namna ya kuhawilisha maneno haya yakasomeka kisanii zaidi. Pamoja na kuwa matini hii ni ya kifasihi, mwandishi na mfasiri wameingiza istilahi za kidini.

Kadhalika, waandishi wengine wamejitalidi kuiga kwa karibu lugha hiyo katika uandishi wa matini nyingine zinazozungumzia masuala ya uwanja wa dini. Mnyampala (1963), kwa mfano, katika mashairi yake kuhusu Yohana (10, 11-18) na Mathayo (5, 3-12) ameandika:

**Mchungaji Mwema**

Yohana (10, 11-18)

1. Mimi ni mchunga mwema.  
Ni mchungaji wa kweli,  
Sina hofu najituma,  
Kwa kifo na minajili.  
Mchungaji kondoo mwema.  
Hawamo na wale mbali.  
Si mchungaji wa mali,  
Wa mishahara kulipwa,...
3. Mimi ni mchunga bora.  
Na wachunga kila hali,  
Nawatambua kwa sura,  
Wa kwangu nawataili,  
Na wao wanani dara,  
Nami pia nawajali,  
Wanisikia kauli,  
Nami uzima natowa.

**Wenye Kheri**

Mathayo (5, 3-12)

1. Akamwambia wa kheri,  
Hao walio fakiri,  
Wake wakisubiri,  
Raha watajipatia,
2. Wale wasikitikao,  
Na wale wasumbukao,  
Ndio watukuzwao,  
Faraja itawajia...
4. Na hao wenye huruma,  
Ambao watasi mama,  
Na wapate uzima,  
Mungu tawahirumia.

Mashairi haya ni mwigo wa istilahi na misemo ya kidini. Knappert katika utangulizi wa mashairi haya anasema ni utunzi mpya katika Kiswahili ambao unaeleza masuala ya kidini kwa mtindo wa kishairi. Nyerere pia ameandika tenzi tano kutoka Mathayo, Marko, Luka, Yohana na Matendo ya Mitume. Haya yote yamewezekana kwa sababu ya jitihada za awali za kufasiri maandiko matakatifu na kuunda istilahi za kidini.

**4.0 Hitimisho**

Suala la uzingatiaji wa vipengele vya kimuundo vinavyojitokeza katika aina fulani za matini wakati wa zoezi la kutafsiri, kwa ujumla, ni jambo ambalo hatuwezi kulipa kisogo. Suala hili lina mchango mkubwa sana katika LL kwa ujumla, na katika kuhawilisha maudhui ya matini husika. Aidha, uhawilishaji wa vipengele vya kimuundo husaidia kuipa tafsiri vionjo vinavyowiana na vile vya matini ya LC. Wafasiri katika jitihada za kuvihawilisha vipengele vya kimuundo, huwasaidia waandishi wengine katika lugha lengwa kuiga mbinu hizo na kuandika matini za aina fulani.

**Marejeo**

- Biblia Maandiko Matakatifu (1997), Dodoma: The Bible Society of Tanzania  
 Damman, E (1977), Some Problems of translation of the Bible into African Languages. Katika *Kiswahili*, Juz. 47/2, 88-95  
*Endagano Empya N'Zaburi*. 1968/1972. Nairobi: United Bible Societies.  
 King'ei, K (2002), The Challenge of Translating Poetic and Metaphorical Language from a Translation: The Case of Okot p'Bitek's *Song of Lawino*. In *Metamorphoses Journal*. Massachusetts: Amherst/ Northampton, Juz. 10, Na. 1, 152-163

- Malangwa, P.S (2005). Problems of Translating Literary Works: The Case of Julius Kambarage Nyerere's Translation of the Play *Mabepari wa Venisi*. Unpublished M. A. Dissertation, University of Dar es Salaam
- \_\_\_\_\_. (2008). Ukiushi katika Kutafsiri Matini za Kifasihi: Misano kutoka Tafsiri ya Julius Kambarage Nyerere ya Mabepari wa Venisi. Katika *Kiswahili Journal* Na. 71, 24-33
- Mapaje, L. & L. White. (1983). *Oral Poetry from Africa*. Essex: Longman
- Mnyampala, M.E. (1963), Two Versification of the Gospel. Katika *Kiswahili*, Juz.33/2, 24-25
- Mojola, A (1999), *God Speaks in Our Own Languages*: Dodoma: Dodoma Bible Society of Tanzania
- Mwansoko, H.J.M, R.D.K Mkeacha, D. L.W Masoko & P.C.K Mtesigwa. (2006). *Kitangulizi cha Tafsiri: Nadharia na Mbini*. Toleo la Pili, Dar es Salaam: Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili
- Mwita, G. J (2008), Mchango wa Wamisionari wa Kikristo na Shirika la SIL International katika Maendeleo ya Lugha za Tanzania. Katika *Occasional Papers in Linguistics*. Dar es Salaam: Mradi wa Lugha za Tanzania, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Na. 2, 41-50
- Nyerere, J. K (1996). *Utenzi wa Matendo ya Mitume*. Peramiho: Ndanda Mission Press
- \_\_\_\_\_. (1996). *Utenzi wa Injili ya Mathayo*. Peramiho: Ndanda Mission Press
- \_\_\_\_\_. (1996). *Utenzi wa Injili ya Yohane*. Peramiho: Ndanda Mission Press
- \_\_\_\_\_. (1996). *Utenzi wa Injili ya Marko*. Peramiho: Ndanda Mission Press
- \_\_\_\_\_. (1968), *Mabepari wa Venisi*. Dar es Salaam: Oxford University Press
- Ohly, R (1975), The Translation of Bible into African Languages. Katika *Kiswahili*, Juz. la 46/1, 82-84
- Savory, T.H (1968), *The Art of Translation*. London: Jonathan Cape
- Shakespeare, W. (1987), *The Merchant of Venice* by M.M. Mahood (Ed.). Cambridge: Cambridge University Press
- Tenzi za Rohoni (1968), Musoma: Musoma Press
- The Holy Bible (1973), USA: New International Version